BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tatu – Tarehe 30 Novemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

101. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwenye suala la mazingira, miti ni kitu muhimu sana katika kuhifadhi, kuzuia mimong'onyoko ya ardhi na masuala ya mabadiliko ya hali ya tabia nchi.

Pamoja na jitihada za Serikali, suala la kupanda miti kwa wingi na suala la kukata miti bado tunalichukulia wepesi kwani bado wapo watu wanaokata miti ovyo. Kupanda miti kwa siku ya mazingira duniani haitoshi.

(a) Je, Serikali inalijua suala la kukata miti kiholela linaongezeka siku hadi siku.

(b) Je, Serikali haioni yapo maeneo mengi sasa tayari yanaelekea kuwa jangwa.

(c) Je, ni mpango upi mahususi wa kuirudisha Zanzibar katika uhalisia wake wa kijani.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

73. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Barabara za ndani ya Jimbo la Tunguu (*feeder roads*) zimekuwa na hali mbaya sana Kwa nini Halmashauri ya Wilaya za Kati isifanye bidii za makusudi kuomba fedha kutoka Serikali Kuu ili ifanye matengenezo ya barabara hizo wakaazi wapate unafuu.

91. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa wapiganaji wa Vikosi vya SMZ na Idara Maalum wanafanyakazi kubwa ya ulinzi wa nchi na pia kushiriki katika kukuza uchumi wa Zanzibar kwa uzalishaji mali katika sehemu zao. Na kwa kuwa Wizara iliombwa na wapiganaji hao katika mikutano yake na kuahidi kuwaongezea posho la chakula tokea mwaka 2016.

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

(b) Je, hatuoni kutotekelezwa kwa ahadi hiyo kuna wavunja moyo wapiganaji wetu.

Wizara ya Fedha na Mipango:

67. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Nampongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika juhudi zake za kuiletea maendeleo Zanzibar na wananchi wake. Hata hivyo, katika

suala la miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali hutokea kuanza vizuri lakini miradi mingi haimalizi kwa wakati.

(a) Je, Wizara inalijua hilo.

(b) Je, Wizara haioni tatizo hilo huzorotesha maendeleo na malengo iliyoyakusudia.

(c) Je, Wizara haioni kusimama au kukwama kwa baadhi ya miradi hiyo ni kuiongezea gharama nyengine Serikali.

Wizara ya Afya:

7. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa muda mrefu sasa Pemba imekuwa haina Bohari ya dawa hali inayoleta usumbufu wa upatikanaji wa dawa kisiwani humo.

Je, ni lini Serikali itajenga Bohari ya dawa kisiwani Pemba ili kurahisisha upatikanaji wa dawa Pemba.

.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

11 MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Kumekuwa na mpango wa Serikali kuweka wakala wa kununua sukari ya Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kupitia wafanyabiashara kununua tani karibu 4,000 na zilizobakia waagize kutoka nje. Bei ya sukari inayoagiziwa kutoka nje ni shilingi 65,000/=, wakati sukari watakayonunuwa mawakala Kiwanda cha Mahonda na nyengine watakayoagiza inadaiwa watauza kwa shilingi 95,000/=.

(a) Je, Mpango huo upo kweli kama hivyo.

(b) Je, ni kigezo gani kimetumika kwa wafanyabiashara hao kupewa uwakala wa kununua sukari ya ndani na ya nje na kuuza kwa bei ya juu kutoka 65,000/= hadi 95,000/=.

(c) Je, Serikali haioni kuwa mpango huo unakwenda kinyume na Sheria ya Biashara kwa Kuzuwia ushindani wa biashara (uncompetitiveness)na kuwaumiza wananchi.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

52. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Hivi karibuni Serikali iliandaa kamati maalum ya kuongoza ZFA katika kipindi cha mpito. Miongoni mwa kazi ambayo kamati hiyo ilipewa ni kutayarisha Katiba mpya ya ZFA.

(a) Kwa kuwa kamati hiyo ni ya miezi mitano (5), na kwa kuwa baadhi ya kazi ilizopewa zimekwisha malizika, ni lini kamati hiyo itamaliza majukumu yake.

(b) Je, ligi kuu ya Zanzibar ya mwakani itatumia Katiba gani ya ZFA.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

19. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Benbella imeshika mkia katika skuli kumi (10) zilizofanya vibaya katika matokeo ya kidato cha sita (6).

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani baada ya matokeo hayo mabaya.

(b) Skuli hii ina walimu wa kutosha, vifaa na maabara tofauti na skuli ya Mtule, Je, ni nini chimbuko la kufanya vibaya.

(c) Je, Wizara inatoa kauli gani kwa wanafunzi waliokuwa hawakufanya vizuri.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

24. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwa kuwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliwapeleka masomoni wafanyakazi 99 kwa muda mrefu jambo ambalo ni zuri na la kupigiwa mfano kwa Wizara nyengine.

(a) Je, Serikali ilitumia kiasi gani cha fedha kuwalipia wafanyakazi hao kwenye vyuo wanavyosoma.

(b) Je, ni wafanyakazi wangapi wanasoma katika vyuo vya ndani ya Tanzania na wangapi wanasoma vyuo vya nje ya Tanzania.

(c) Je, Wizara ina jumla ya wafanyakazi wangapi kwa Taasisi zake zote.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

47. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni Wizara yenye wataalamu wengi hasa katika fani ya kilimo. Na kwa kuwa wakulima wengi hasa wanawake wanalalamikia uelewa mdogo wa utaalamu wa kuendesha shughuli zao za kilimo.

(a) Je, wataalamu hawa wa kilimo wanatumia vipi utaalamu wao kuhakikisha wanawasaidia wakulima hasa wanawake ili waweze kuingia katika soko na kulima kilimo cha biashara na kuepuka kilimo cha mazoea.

(b) Ni kwa vipi wataamu hawa wameweza kuwashajihisha vijana ili waweze kushiriki katika kilimo cha biashara na hatimae kuondokana na hali ngumu ya umasikini.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

36.. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kuwa moja ya kazi ya biashara ya Makampuni ya Ndege kote ulimwenguni ni kubeba abiria na mizigo ama kufuatana na abiria mwenyewe au "*parcels*". Lakini kwa viwanja vyetu vya Zanzibar Makampuni ya ndege yanayobeba abiria kutoka viwanja vyetu vya ndani yamezuiwa kubeba mizigo isiyofuatana na abiria.

(a) Je, ni sababu gani iliyopelekea Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ikayazuia Makampuni hayo kusafirisha "Parcels" au mizigo ya watu ambao si abiria.

(b) Je, ni sheria gani ambayo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege waliyotumia ili kuzuia utumaji wa mizigo midogo midogo au "parcel" zisitumwe kupitia ndege zinazokwenda Pemba au sehemu nyengine za ndani ya Tanzania.

(c) Je, Mamlaka haioni kwamba kuzuia kusafirisha mizigo midogo na "parcels" kunawakosesha mapato Makampuni na vijana wetu ambao wanafanya kazi hapo.

86.. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika malengo yake ya mwaka 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni kujenga bandari ya Mpigaduri.

(a) Je, suala hili limefikia wapi.

(b) Je, ni lini ujenzi huo utaanza.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
30 Novemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.